N10/2/ABSWA/HP1/SWA/TZ0/XX/T

88102388

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Tuesday 2 November 2010 (morning)
Mardi 2 novembre 2010 (matin)
Martes 2 de noviembre de 2010 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

8810-2388

6 pages/páginas

© International Baccalaureate Organization 2010

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**



# BILA NDURURU HUNUNUI CHOCHOTE!

Utasikia mtu akikuambia eti ndururu haina thamani lakini hebu ikose hiyo ndururu halafu uone ikiwa utanunua kitu chochote kutoka dukani. Nilipokuwa mtoto mdogo wazazi wangu walipenda kunituma dukani kununua vitu vya kutumia nyumbani. Nyumbani kwetu hatukuwa na mazoea ya kununua vitu kwa jumla, tulinunua vitu tulipovihitaji tu na katika vipimo vidogo vidogo. Tulifanya hivyo kwa sababu hatukuwa na namna bora ya kuvihifadhi na pia haikuwa katika utamaduni wetu kununua vitu vingi ambavyo hatukuwa na haraka ya kuvitumia.

Jambo ambalo ninakumbuka wazazi wangu wakinikumbusha kila waliponituma dukani ni kuwa ilikuwa ni lazima nirudishe chenji. Wazazi wangu waliamini kwamba kila senti ilikuwa muhimu. Mama alikuwa na mahali alipokuwa akiiweka kila chenji tuliyorudisha. Sote katika familia tuliamini kwamba “akiba haiozi na kidogo kidogo hujaza kibaba.”

Wakati mmoja nilipokuwa katika shule ya upili, mama alitaka kuona akiba yake ya chenji ile ya ndururu, thumni, peni na hata shilingi moja moja iliyokuwa ikikusanywa kwa muda mrefu. Mama aliukata mkebe ambao alikuwa ameuweka mvunguni mwa kitanda. Mkebe huo ulikuwa mzito sana. Aliuweka juu ya meza na kumwaga chini vitu vyote vilivyokuwemo. Amini usiamini baada ya sarafu hizo zote kuhesabiwa idadi ya pesa zilizopatikana ilikuwa elfu ishirini. Kwa hivyo, ikiwa unataka kuwa tajiri, anza kudunduliza kila ndururu unayorudishiwa kama chenji unapoenda dukani au sokoni.



A Omar, *et al.*, (2007), Tuwasiliane kwa Kiswahili, NARLC Press, Wisconsin-Madison



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**


# SIKU ZA SOKO KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI



Katika Afrika ya Mashariki, bidhaa hupatikana katika sehemu nyingi sana. Kuna watu ambao wanauza bidhaa zao mitaani, kuna wale ambao wanaziuza vibandani, kuna wale wanaziuza katika masoko wazi, na kuna wale ambao wanaziuza katika maduka madogo na makubwa vijijini na mijini. Pia, katika baadhi ya sehemu kuna siku maalum kwa vitu maalum. Kwa mfano, ikiwa mtu anataka kununua ng'ombe au nyama kuna siku maalum ambazo zimetengewa uuzaji wa ng'ombe na pia siku maalum ambapo wenye vichinjio hununua na kuwachinja ng'ombe. Kuna hata masoko maalum ya mbwa katika baadhi ya sehemu za nchi kwa mfano, huko Kakamega, mahali panapoitwa Lubao nchini Kenya kuna soko maalum la kuuza mbwa na watu husafiri kutoka sehemu mbalimbali kwenda kuwatafuta mbwa wanaowapenda.

Kwa kawaida kila sehemu huwa na siku ya soko. Watu kutoka sehemu mbalimbali hukusanyika na kuanza kuuza au kunadi bidhaa zao. Wateja nao hutoka sehemu mbalimbali ili kujipatia bidhaa mbichi kama nguo, pia wateja huzipata kwa bei nafuu ikilinganishwa na bidhaa za maduka makubwa mijini.

Wafugaji huamka usiku wa manane ikiwa wanaishi mbali na soko ili wawahi kufika sokoni kabla ya jua kuchomoza na kuwa kali. Wao wanaamini kwenye msemo "ajaaye kisimani mbele hunywa maji maenge". Mifugo yao ambayo sana sana huwa ng'ombe, mbuzi na kondoo, hutembezwa hadi sokoni ambako wateja nao pia huamka mnamo saa kumi na moja alfajiri ili wawapate wanyama wa kufuga wenye afya na wale ambao wanaweza kuwaletea faida kwani "ukitaka kula nguruwe chagua aliyenona". Ni mahali kama hapa ambapo watu wenye vichinjio huenda ili kupata wanyama wa kuchinja.



Kwa ufupi basi, mtu yeyote anayetaka vyakula ambavyo ni vya bei nafuu na vile ambavyo bado vina ubichi wake wa kutoka shambani anahimizwa kuyatembelea masoko haya ambayo hupangwa kutegemea siku za juma. Kwa mfano, siku za soko katika kituo fulani cha biashara au mji fulani zinaweza kuwa Jumatano, Jumamosi au Jumanne na Alhamisi. Idadi ya siku za soko katika juma kwa kawaida hutegemea ukubwa na umaarufu wa kituo hicho cha biashara.


Taifa Leo, Novemba 2009



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

# HAZINA BORA



Kijiji cha Kivumbini kilipakana na Gongo la msitu. Tulikitokezea kijiji hiki kwa ghafla. Mimi pamoja na marafiki zangu Matufu na Matule, tulifurahi ukomo wa kufurahi. Watu wa Kivumbini walikuwa maarufu sana kwa ukarimu wao. Tulibisha nyumbani mwa bwana mmoja jina lake Matambo. Alitukaribisha kwa mikono miwili. Nyumba yake ilikuwa ya kimaskini. Mwenyewe alikuwa kavaa mararuraru yaliyotangaza uchochole wake. Lakini kama wasemavyo wahenga "Kutoa ni moyo usambe ni utajiri".

Tuligundua punde kuwa alikuwa kafiwa na mkewe hivi karibuni. Lakini hakujisononesha kuliko ilivyokuwa lazima. Alituandalia malazi kwa fadhili. Kulipopambazuka akaandika kiamshakinywa mezani. Tulipokuwa tunastaftahi alianzisha mazungumzo ghafla.

"Mlionekana wachovu sana mlipokuja hapa jana. Ilionekana mlitoka safari ya mbali?" aliuliza yule bwana.
"Ndiyo," akajibu Matule.
"Mlitoka wapi?" akauliza tena.

Nikamgeuzia macho Matufu. Akaangalia kando. Kimya. Moyo wangu ukapigapiga kwa kasi. Nikaangalia chini. Mfadhili wetu alipoona tunatapatapa aligeuza mazungumzo.

"Nilikuwa nikimpenda sana mke wangu azizi Saida. Lakini sijaomboleza peke yangu. Watu wa mbali na wa karibu walifika matangani. Babu yake Saida pia alikuja. Amelia kutwa kucha tangu alipowasili. Anasema maisha ya Saida yamekatika angali mdogo. Babu yake ni mkarimu na mwerevu sana.



https://xtremepape.rs/

Je, anajua kufumbua mafumbo magumu?" alisaili Matule.

"Kama lipi?" aliuliza Matambo.
"Kama kitendawili changu ambacho kimewashinda wengi kukitegua," alijigamba Matule.
"Aah! Kitendawili gani? Hata mimi sishindwi na kitendawili. Tega! Alinena Matambo.
"Ninayo hazina bora isiyoweza kununulika kwa pesa?"
"Lahaula! Kwa kweli mimi sijui.


Lakini sauti yake ilikatishwa na mchakacho wa miguu pale nje. Punde si punde, mtu akaingia ndani pasi kubisha. Tuliduwazwa na mjo wake. Miguu ilitutetemeka. Mbele yetu akazuka Mzee Mataka.
"Shikamoo babu," mwenye nyumba alimwamkua kwa adabu.

"Marahaba Matambo," akajibu Mzee Mataka. "Basi nipeni kiti nitegue kitendawili."
"Hazina bora isiyoweza kununulika kwa pesa ni adabu njema. Walakini adabu njema siku hizi," imeadimika. Wazee wamekuwa mfano mbaya nao vijana wanafuata tabia zao.
Jasho jembamba lilitutoka vipajani and Matule alianza kulia.
"Tuwie radhi sana babu… tumekukosea. Tuliiba maembe yako… ulipo…"
"Nyamaza bwana mdogo. Yaliyotokea Bombani baada ya mimi kuondoka nayajua yote.

Yule msichana Fatuma aliyeanguka kutoka mwembeni anaendelea kupata nafuu. Alipata majeraha madogo. Hofu ilikuwa kwenu. Watu wa Bombani watafurahi kuwaona.

Madhali mmepatikana yamekwisha haya. Mkirudi Bombani muwe na adabu njema.

Siku hiyo Mzee Mataka aliambatana nasi hadi Bombani. Alitulipia nauli na kugharamia masurufu. Alituusia mengikuhusu maisha. Watu wa Bombani walikuwa radhi kutusamehe. Fatuma alithibitisha kuwa hakusukumwa na yeyote kutoka mtini. Baada ya matibabu, alirudi shuleni and kukiri kuwa alikosa adabu njema.



Ken, Walibora, (2007), Macmillan publishers, Kenya



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# ATHARI YA MAZINGIRA KWA UKULIMA NCHINI TANZANIA



Kilimo ni uti wa mgongo nchini Tanzania and watu wengi hukitegemea mno. Kilimo kimewasaidia wananchi wengi kujipatia vyakula vya kutosha kwa matumizi na vingine kuviuza kupata pesa kwa matumizi mengine. Baadhi ya mazao ya chakula yanayolimwa na wakulima ni ndizi, mahindi, mihogo, mboga, mpunga, ngano, nazi na matunda. Wakulima pia hulima mazao ya biashara kama vile kahawa, chai, pamba, korosho na karafuu. Mazao haya yakiuzwa huwapatia wakulima pesa za kutumia kwa matumizi yao mbalimbali kama vile kulipa karo, kununua mavazi na kujenga nyumba.



Kufanikiwa kwa ukulima nchini Tanzania kunategemea hali ya mazingira. Wakulima nchini Tanzania wamekuwa wakikumbana na matatizo mbalimbali ya kimazingira. Matatizo haya hudhoofisha kilimo na husababisha ukosefu wa vyakula kwa wafanyakazi wa mjini na pia kwa wakulima. Baadhi ya matatizo haya ni suala la mmomonyoko wa udongo. Tatizo hili huwepo mvua inaponyesha sana na maji kuuondoa udongo mzuri wenye rutuba. Mvua nyingi husababisha mafuriko makubwa yanayochukua udongo wenye rutuba na hata mazao. Katika sehemu zenye joto kama vile Dodoma, jua kali husabisha ukame na hukausha mazao. Katika maeneo hayo kuna upepo mkali ambao hupeperusha udongo wa juu na kuuacha wa ndani usio na rutuba. Sehemu zenye mifugo mingi kama Umasaini, mifugo husababisha mashimo kwenye njia wapitazo kila siku. Mashimo hayo huleta mmomonyoko wa udongo.

Dhoruba ni tatizo jingine kubwa ambalo husababisha madhara katika kilimo. Mara nyingi dhoruba huja na mvua kali na upepo huangusha mazao mengi kama ilivyo kila mara kwenye mkoa wa Kagera. Upepo huo mara nyingi huja wakati mvua ya mawe ikinyesha. Matatizo mengine ni ya wadudu na wanyama waharibifu. Matatizo haya hupunguza kiwango cha mazao yanayozalishwa na faida za ukulima.

Ili kupambana na matatizo ya kimazingira, wakulima wengi wamekuwa wakishauriwa kuyatunza mazingira ili yawe bora kwa kilimo. Kwa mfano, wanashauriwa kufunika mashamba yao kwa kutumia nyasi ili maji au upepo usimomonyoe udongo wa juu wenye rutuba. Wanashauriwa pia kutunza udongo kwa kuweka matuta ya kuyakinga maji. Pia wanaelezwa umuhimu wa kuchimba mifereji ili maji yapate kupita, kutumia madawa ya kuua wadudu, kupanda miti, kuhifadhi misitu na kuweka mbolea katika mazao yao.

Mzalendo, Novemba 2009



https://xtremepape.rs/